

KILIMO BORA CHA APPLE

Rababa Imani
Oktoba 02,2017

UTANGULIZI(*Malus pumila*)

Apple ni moja kati ya matunda yanoyo pendwa sana, na wengine wamefikia mbali hadi kulifanya apple kua tunda la ishara ya upendo, pia kuna aina mbili za matunda ya apple yaani yanoyo liwa bila kupikwa na yale ambayo ni lazima yapikwe ili uweze kuyala.

Matunda ya apple hayafanyi vizuri katika maeneo ya joto, huitaji hali ya hewa iliyo tulia na isio kua na joto kali, kutokana na mahitaji haya apple hukua vizuri Tanzania kwenye maeno ya umbali wa 2000- 3000 meters kutoka usawa wa bahari. mfano Mbeya, Arusha na Iringa.



AINA
Aina
nyingi
za
apple

www.tanzanianakilimo.blogspot.com

hutegemea miti ya aina nyingine iliyo pandwa karibu ili kuwezesha kuichavusha(pollination) hivyo mkulima ni lazima kupata ushauri kutoka katika office za mboga mboga na matunda(holiticultural) ili kuweza kupata aina nzuri zaidi.

kwa Tanzania utafiti wa apple hufanywa katika kituo cha uyole kilichopo Mbeya na kituo cha Tengeru kilichopo Arusha unaweza kupata aina nzuri zaidi kutoka katika hizo taasisi.

JINSI YA KUPANDA

kwa kawaida miche ya apple upatikana kwa kutumia njia ya grafting na unaweza kupata miche hiyo katika taasisi binafsi au za serikali nilizo zitaja hapo awali.
nafasi ya upandaji inategemea na aina ambayo unataka kupanda]

1. aina ndogo 2m x 2m
2. aina ya kati 2.5m x 2.5m
3. aina kubwa 3.0m x 3.0m

KUANDAA SHAMBA

Kama ardhi unayo panda inamtemeko ni lazima ufate mistari ya kontua, pia chimba mashimo ya kupandia kila shimo linatakiwa kua na 60cm upana na 60 cm urefu.



KUPANDA

Miche ambayo imekuzwa katika kitalu inatakiwa kuiamishia shambani katika kipindi ambacho hakuna joto, lakin miche ambayo imekuzwa kenywe poti au karatasi za plastik zinaweza kupandwa mda wowote ule.

unapopanda panda katikati ya shimo na hakikisha mizizi yote umeitandaza, changanya udongo wa juu(top soil) na ndoo mbili za 20 liters za mbolea ya samadi,na baada ya kupanda hakikisha unamwagilia vizuri.

kama aina yako inaitaji kuchavushwa basi hakikisha unapanda miche ya uchavushaji kila baada ya mistari 2 au 3 ya aina ambayo unataka kuchavushwa.

KUKATIA (PLUNNING)

Miti ya apple inaitaji sana kupruniwa katika miaka 3 ya kwanza ili kuweza kukua vizuri na kutengeneza umbo lililo zuri.

baada ya miaka 3 na mti umeshakua na umbo linalo itajika unacho takiwa ni kupluni au kukata matawi yaliyo vunjika, yaliyo kauka au yaliyo kua nje ya utaratibu.

MBOLEA

Kama mbolea ya samadi au mboji inapatikana unatakiwa kuweka liter 20 za mbolea katika kila mche kwa kila mwaka pia DSP na CAN au SA inaitajika kwa kila mwaka. unaweza kuwasiliana na afisa ugani wa eneo lako ili kupata ushauri zaidi.

KUVUNA

matunda hua madogo pale yanapo kua na msongamano, ili kuepusha hilo zingatia kuvuna matunda yote yanayo kua yamekomaa ili kuyapa n afasi mengine.

MAGONJWA NA WADUDU WAHALIBIFU

Wadudu wahalibifu ni

- wooln aphids
- bui bui wekundu
- mchwa

magonjwa

- ubuli unga
- kuoza mizizi
- apple anker
- apple scab

unaweza kuzuia kwa kutumia dawa za wadudu au wasiliana na afisa ugani aliyo karibu nawe.



www.tanzanianakilimo.blogspot.com

Imepakuliwa tarehe 11/12/2023

Inapatikana www.tanzanianakilimo.blogspot.com